

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>
Unapojibu tafadhali taja:



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi
S.L.P. 670,
DODOMA.

Kumb. Na. CAC 17/228/01/A/169

24 Mei, 2022

Makatibu Wakuu Wote,
Katibu wa Bunge la Tanzania,
Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania,
Wakuu wa Idara zinazojitegemea wote,
Makatibu Tawala wa Mikoa wote,
Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali,
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji Wote,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya wote,
TANZANIA BARA.

Kuh: WARAKA WA WATUMISHI WA UMMA NA. 1 WA MWAKA 2022

KUHUSU POSHO YA KUJIKUMU KWA SAFARI ZA KIKAZI NDANI YA NCHI

Tafadhali rejeeni somo la hapa juu.

2. Pamoja na barua hii ninawaleteeni Waraka wa Watumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2022 kuhusu Posho ya Kujikimu kwa Safari za kikazi ndani ya nchi

kwa ajili ya utekelezaji na kumbukumbu ya Ofisi zenu. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2022.

Ninawatakia utekelezaji mwema.

A. K. Meena

Kny: **KATIBU MKUU (UTUMISHI)**



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670,
DODOMA.

Kumb. Na. CAC 17/228/01/A

24 Mei, 2022

WARAKA WA WATUMISHI WA SERIKALI NA. 1 WA MWAKA 2022

KUHUSU POSHO YA KUJIKIMU KWA SAFARI ZA KIKAZI NDANI YA NCHI

UTANGULIZI

1. Viwango vinavyotumika sasa kwa ajili ya posho ya kujikimu kwa safari za kikazi ndani ya nchi viliwekwa kupitia Waraka wa Utumishi Na. 4 wa mwaka 2014 kuhusu Posho ya Kujikimu Kwa Safari za Kikazi Ndani ya Nchi. Kwa kuzingatia kupanda kwa gharama za maisha, Serikali imefanya marekebisho ya viwango vya posho ya kujikimu kwa safari za kikazi za ndani ya nchi.

HADHI YA MIJI

2. Kwa madhumuni ya ulipaji wa posho ya kujikimu, hadhi ya miji na sehemu nyingine zimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:
 - i. Jiji na Manispaa;
 - ii. Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya; na
 - iii. Sehemu nyingine.

VIWANGO VIPYA VYA POSHO

3. Viwango vipya vya posho ya kujikimu vitakuwa kama ifuatavyo:

Na.	Ngazi za mshahara	Jiji na Manispaa (Shilingi)	Miji Mikuu ya Mikoa na Miji Mikuu ya Wilaya (Shilingi)	Sehemu Nyingine (Shilingi)
1.	LSS (J) 1 - LSS (J) 3, LSS (E) 5 - LSS (E) 9, LSS (P) 1 - LSS (P) 6.	250,000	200,000	130,000
2.	LSS (E) 1 - LSS (E) 4	220,000	180,000	120,000

Na.	Ngazi za mshahara	Jiji na Manispaa (Shilingi)	Miji Mikuu ya Mikoa na Miji Mikuu ya Wilaya (Shilingi)	Sehemu Nyingine (Shilingi)
3.	TGS F - TGS I, TGTS G - TGTS J TGHS E - TGHS L, TJS 4 - TJS 6, AGCS 4 - AGCS 13, TGRS C - TGRS I, PSS F - PSS L, SAIS F - SAIS Q	170,000	150,000	100,000
4.	TGS C - TGS E, TGTS C - TGTS F, TGHS B - TGHS D, TJS 1 - TJS 3, AGCS 2 - AGCS 3, TGRS A - TGRS B, PSS C - PSS E, SAIS C - SAIS E	150,000	130,000	80,000
5.	TGS A - TGS B, TGOS A - TGOS C, TGHOS A - TGHOS C, PSOS A - PSOS C, TGTS B, TGHS A, AGCS 1, PSS A - PSS B, SAIS A - SAIS B	100,000	80,000	70,000

GHARAMA ZA SAFARI NJIANI (ON TRANSIT)

4. Mtumishi wa Serikali anapokuwa njiani (on transit) kwa safari ya saa sita (6) au zaidi/nje ya mkoa ambao kituo chake cha kazi kipo atapewa asilimia hamsini (50%) ya posho ya kujikimu kwa siku kwa kiwango cha mahali anapokwenda kwa ajili ya matumizi ya njiani.

POSHO YA KUJIKIMU KWA AJILI YA MTOTO

5. Endapo itatokea ulazima wa Afisa kusafiri na mtoto mdogo asiyezidi miaka mitatu (3), asilimia hamsini (50%) ya kiwango cha posho ya Afisa (Mzazi) itaongezwa kwa ajili ya kumgharamia mtoto.

KIBALI CHA KUFIKIA HOTELI YA GHARAMA YA JUU KULIKO KIWANGO CHA POSHO YA KUJIKIMU

6. Madhumuni ya Serikali kuongeza viwango vya posho ya kujikimu ni kuwapa nafuu watumishi wake na wakati huo kupunguza matumizi ya fedha za Serikali kwa kuwataka watumishi waishi katika Hoteli za gharama nafuu.
7. Hata hivyo, inapotokea kwa sababu za kikazi Kiongozi/Viongozi kulazimika kufikia katika Hoteli ambayo gharama zake ni kubwa kuliko posho ya kujikimu, Afisa Masuuli anaweza kufanya moja kati ya mambo yafuatayo:-
 - i. Kumlipia/kuwalipia kikamilifu (full board) gharama za malazi na chakula bila ya fedha ya ziada; au
 - ii. Kumlipia/kuwalipia gharama za malazi (half board) pamoja na kulipa nusu ya posho ya kujikimu kwa ajili ya kugharamia chakula.

KUDHIBITI MATUMIZI

8. Kila Afisa Masuuli anatarajiwa kulipa viwango vipya vya posho kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa katika bajeti yake kwa mwaka husika. Hivyo, ni wajibu

wa Afisa Masuuli kuzingatia viwango hivi na kudhibiti safari zinazofanywa na maafisa walio chini yake ili kuepusha safari zisizokuwa na umuhimu.

MENGINEYO


9. Viwango vipya vya posho ya kujikimu vitatumika pia kwa Wakala na Taasisi za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma yanayopata asilimia mia moja (100%) ya ruzuku ya Serikali. Aidha, Mashirika ya Umma yanayoendesha shughuli zake kibiashara yataingatiwa viwango vya posho ya kujikimu na Msajili wa HAZINA na kupata idhini ya Katibu Mkuu - Utumishi kabla ya kuanza kutumika.

TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

10. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2022 na unafuta Waraka wa Utumishi Na. 4 wa mwaka 2014 kuhusu Posho ya Kujikimu Kwa Safari za Kikazi Ndani ya Nchi.

MWISHO

11. Waraka huu ni kumbukumbu na taarifa ya Serikali na hairuhusiwi kutangazwa kwenye vyombo vya habari.



Dkt. Laurean J.P. Ndumbaro

KATIBU MKUU (UTUMISHI)